For more visit : eazyarabic.com



## SEHEMU A: TAMTHILIA

(a)

i. Haya ni maneno ya Boza.

ii. Anamwambia Kombe.

iii. Wako kwenye karakana, sokoni Chapakazi.

iv. Kombe amemwuliza kama mkewe Boza amepata kandarasi ya kuoka keki ya kusherehekea miaka sitini ya uhuru, ndipo Boza anamjibu hivi.

**Hoja 4 x 1 =** *(alama 4)*

**Tanbihi**

Dondoo limetolewa uk. 7

(ii)

i. Swali la balagha – Aikose? – Kuonyesha kwamba hawezi kukosa. Kujivunia weledi wa mke wake.

ii. Uashiriaji/ – Matumizi ya neno 'hapa' yanaonyesha mtu anamweleleza mahali/kwenye sehemu ya mwili.

iii. Ulinganuzi – anaonyesha mkewe kama anayempiku Husda kwa ulaghai/akili. Amemweka Husda hapa( kwapani)

iv. Taswira

- hapa – taswira mwendo.
- halisi – taswira mguso

v. Nidhaa – Mwanamke halisi bwana!

Hoja 2 x 1 **(alama 2)**

Kutaja-1

Mfano-1

(iii) Anayeambiwa ni Kombe

i. Mwenye utani - Anamtania Boza kwa kumwambia kuwa anagaragara kama kuku anayetaka kutaga (Uk. 1).

ii. Mtambuzi – anayatambua masaibu yanayowakumba.

iii. Mdadisi – anataka kujua sababu ya sherehe kuwa mwezi mzima.



Scanned with CamScanner

iv. Mwenye busara – anakisia kuhusu hali itakavyokuwa iwapo sherehe itakuwa ya mwezi mzima.

v. Mwenye stihizai – anamwita Sudi Professa wa siasa. Anawaliza Boza na Sudi kwa kejeli, iwapo hawajasikia kuwa kunasherehekewa uhuru( uk.6).

vi. Mpatanishi – anawatuliza Boza na Sudi wanapokabiliana.

vii. Mwenye bidii – Yeye na wenzake wanachonga vinyango kwa madhumuni ya kuzikimu familia zao.

**Hoja 4 x 1** **= alama 4**

**Kutaja- 1/2**

**Mfano- 1/2**

b)

(i) Uzinifu wa Majoka unapalilia mgogoro kati ya Husda Ashua. Majoka anawakutanisha ofisini,wanapigana.

(ii) Tendo la Majoka la kumtaka Ashua mapenzi na kumkejeli kwa kuolewa na mume asiyeweza kuikimu familia yake kunamfanya Ashua amkosee mumewe heshima. *Anamwambia Sudi anahitaji matunzo* (uk 47). Anamwambia kuwa amechoka *kupendwa kimaskini* (uk 47). Ashua anamtisha Sudi kwa kudai talaka( uk.47).

*(iii)* Uzinifu wa Majoka unasababisha mgogoro baina yake na Husda.

*(iv)* Ukosefu wa uwajibikaji katika ndoa unazorotesha mahusiano ya kiunyumba kati ya Majoka na Husda. Majoka anamwoa Husda ili kutimiza matakwa ya jamii na anaishia kumdhalilisha. Anasema hampendi, hakumpenda na hatampenda (uk 75). Anaishi na Husda kiwiliwili tu.

(v) Unyakuzi wa mali ya umma (Soko la Chapakazi) unaathiri uhusiano kati ya uongozi na raia. Tunu na Sudi wanaungana na vijana wenzao kuUondoa uongozi wa Majoka.

(vi) Mauaji yanayotekelezwa na viongozi yanazorotesha uhusiano kati ya viongozi na wapiganiaji haki pamoja na raia. Tunu anahisi uchungu kwa kuuawa kwa baba yake.

*(vii)* Uongozi kukosa kuwajibikia maslahi ya wanyonge kunakuza mgogoro kati ya viongozi na raia. Sudi analalamikia kukusanywa kwa kodi bila kushughulikia usafi wa soko ambamo wanafanyia kazi.



Scanned with CamScanner

(viii) Ukosefu wa uaminifu wa vijana kwa vijana wenzao unaleta kutoelewana kati yao. Kwa mfano, Ngurumo anatumiwa na Majoka kumpiga na kumuumiza Tunu (uk. 63) anamtisha Tunu.

(ix) Ukosefu wa uwajibikaji wa Mamapima kuwauzia vijana pombe haramu unazua kutoelewana kati yake na vijana wapigania haki kama vile Tunu. Tunu analalamikia vifo vya vijana kutokana na pombe hii. (uk. 63)

(x) Ukosefu wa mwelekeo thabiti kuhusu maisha unawafanya vijana kutoelewana. Ngurumo na Boza hawaoni ubaya wowote wa kuuzwa kwa pombe haramu ilhali Tunu na Sudi wanapinga haya. Sudi hapendezwi na tendo la Mtu I kumwongezea Mtu II dozi ya dawa ya kulevya. (uk. 62)

(xi) Ufisadi wa viongozi kunasababisha kutoelewana kati ya wanyonge. Asiya anapewa kandarasi ya kuoka keki kwa sababu ya uhusiano wake na Ngurumo, mumewe Boza anatusiwa kwa kuambiwa kuwa mke wake alioka keki ya uroda (uk 63 – 64).

(xii) Viongozi wanaelekeza kemikali na taka pale ambapo wanyonge wanafanyia kazi. (uk 2) na kusababisha ugomvi kati ya wanyonge. Boza na Sudi wanazozana (uk 2).

(xiii) Kuwaingiza vijana katika utovu wa maadili na thamani za jamii kunaleta kutoelewana/ migogoro kati ya viongozi na raia. Shule ya *Majoka and Majoka Academy* imewatelekeza vijana katika matumizi mabaya ya dawa, hali ambayo inasababisha chuki na kutotosheka kwa wapigania haki. Ashua anabishana na Majoka, anasema hawezi kufanya kazi inayowageuza watoto kuwa makabeji.

(xiv) Jamii kumshinikiza Majoka kuoa ili apate uongozi. Jambo hili linamfanya aishi katika ndoa, asiotaka. Anamsaliti mke wake kwa kuishi naye huku anajua kuwa hampendi. (uk 75).

(xv) Ukaragosi wa Kenga, Ngurumo na Boza kunawafanya wasihusiane vyema na vijana wenzao kama vile Tunu na Sudi.

Hoja 5 x 2 = alama 10

Kutaja - (ukosefu wa maadili)

Kueleza -1 (kuzorota kwa mahusiano)

(xvi) Kufungwa kwa Soko kunawanyima wanyonge mahali pa kutoa riziki

(xvii) Umbeya / uvumi / mafungenyo kunasababisha mgogoro kati ya Sudi na Ashua

(xviii) Ukosefu wa [illegible] wa Majoka / [illegible] kuwatisha raia kwa wiikaretaji vinavyompinga walome vinafanya waishi kwa hofu -

(xix) Kupandishwa kodi kwa bei ya vyakula katika kioski cha kampuni kunasababisha hali duni ya maisha na inawafanya wanateseka [illegible]



Scanned with CamScanner

(xx) Ukataji miti kwa kiongozi Kitwele kunafasalisha kuenea kwa miti na mazingira (ukosefu wa maji).

(xxi) Majoka kumuua Ashua kimapenzi kunachangia kutoelewana kati ya Ashua na Majoka

(xxii) Uzinifu wa Nguruma unamfanya Boza adhihakiwe na Ki...

(xxiii) Tunu/unafasalisha Mgogoro kati ya Boza na Nguruma (uk 63)

**Tanbihi**

Sharti mtahiniwa ataje ukosefu wa maadili/ukiukaji wa haki au thamani za kijamii, kisha aonyeshe mahusiano/uhusiano unavyoharibika ili atuzwe alama 2.

## SEHEMU B: RIWAYA

Tozo 5x2 = alama 10

2.

(i) Wanaendeleza mauaji. Mama yake Sauna anamfanya Sauna kuavya mimba. (uk 155).

- Wanazaa watoto na kuwatupa – Immaculata anaokotwa na Neema kwenye taka.
- Huko kwenye taka pia kunapatikana vijusi vilivyotupwa.
- Wanajiua wenyewe kwa kujiingiza kwenye ulevi – Subira mkewe Kaizari anapatikana amejifia chumbani akiwa na chupa ya kinywaji kikali.

(ii) Wanatelekeza haki ya malezi

- Naomi, mama yake Umulkheri, anawaacha watoto wake kwa kutaka kukimbia umaskini.
- Subira, badala ya kutafuta mbinu za kuishi na mama mkwe, anawaacha Mwanaheri na Lime na kuhamia mjini.
- Mama yake Pete anaolewa na kumwacha; hajali hata kutaka kujua anavyoendelea shuleni.

(iii) Wanachangia katika kuendeleza ndoa za mapema. Mama ya Pete anashirikiana na wajomba wake kumwoza mapema licha ya rai ya bibi yake kwamba wamwache aendelee na masomo (uk 148 – 149).

(iv) Wanaendeleza ulanguzi wa binadamu. Sauna anawateka nyara Dick na Mwaliko, anampeleka Dick kwa Buda. Yeye na Kangara wanawaingiza vijana katika madanguro.

(v) Wanaendeleza ajira ya watoto.

- Sauna anampeleka Dick kwa buda ambapo anaajiriwa.
- Kangara ana mtandao ambapo anawapata vijana na kuwasafirisha baadhi ughaibuni kufanya kazi za kujidhalilisha.
- Pete anamtumia msichana mdogo kumlindia kitoto chake akienda kazini.



Scanned with CamScanner

(vi) Wanaendeleza ubaguzi wa kiukoo. Mamavyaa ya Subira anambagua. Anasema Subira ni msichana wa Bamwezi, anamwona kama asiyeweza kudumu katika ndoa. Anamkosesha utulivu kwa kumwita mwizi.

(vii) Wanachangia kusambaratika kwa asasi ya ndoa. Mavyaa wa Subira anamsimanga Subira hadi Subira anaondoka.

(viii) Wanasababisha dhiki za kisaikolojia. Mkewe Kiriri anamwachia upweke na kwenda ughaibuni. Naomi anamwachia Lunga upweke hadi Lunga anakufa kwa shinikizo la damu.

(ix) Wanahatarisha afya za wengine kwa kuwauzia bidhaa duni. Sauna anawauzia watu maji ya mto yaliyoiwa kwenye chupa za *mineral water*.

(x) Wanawaingiza vijana katika matumizi mabaya ya vileo. Sauna anampeleka Dick kwa Buda ambaye anamtumia kulangua dawa. Dick analazimika kutumia dawa hizo.

(xi) Wanawanyima raia haki ya kuihudumia jamii yao/ kuhudumiwa na jamii yao. Wanachangia uhamiaji ng'ambo wa nguvumali. Sauna na Kangara wanawapeleka vijana ughaibuni wanapofanya kazi za kujidhalilisha.

(xii) Anawanyima haki ya kuishi kiuadilifu. Kuwaingiza wanawake wenzao/wasichana kwenye madanguro – Kangara na Sauna.

(xiii) Wawanyima haki ya kutambuliwa/ kujitambua kama binadamu wenye asili. Kutowaambia kuhusu usuli wao – mamake Pete, hamwambii, mama Kipanga hamwambii kuhusu baba yake.

(xiv) Kuwanyima ushirika na watoto wao- Mkewe Kiriri anahamia ng'ambo na watoto.

**Tanbihi** **10 x 2 = 20**

Sharti mtahiniwa aonyeshe haki inayokiukwa na kuitolea mfano kutoka kwenye kitabu. Aonyeshe mwanamke anayefanikisha ukiukaji huo wa haki za kibinadamu.

3. (a)

i) Kuzungumza moja kwa moja na mzungumziwa ili kufupisha masafa- ujumi kati ya mwandishi/Msimulizi na hadhira. "Una bahati mwenzangu…



Scanned with CamScanner

For more visit : eazyarabic.com

ii) Tashbihi – tulifurushwa kwetu kama taka.

iii) Takriri/uradidi – hujapitia tuliyopitia, tulitendwa ya kutendwa,
Mama, hapo hapo

iv) Tashihisi – amemezwa na njaa na ugonjwa wa udhaifu.

v) Tasfida – alishindwa kukamilisha safari.

vi) Taswira – Tulitanga na njia( taswira mwendo) akaingia kichakani ( taswira mwendo).

vii) Chuku – kilio cha uchungu na jitimai kukihanikiza kote/ kumezwa na njaa

viii) Toni ya huzuni.

ix) Nahau – mezwa na njaa.
- kilio cha uchungu
kitindamimba
roho yake changa ikakatikia hapohapo mgongoni

x) Matumizi ya usemi halisi – "Una bahati sana wenzangu."

xi) Tanakuzi – mbele – nyuma.

xii) Matumizi ya sentensi ndefu.

xiii) Mbinu rejeshi- Kairu anaturudisha nyuma kuhadithia yaliyotokea

(xiv) Kinaya - akina Kairu kufurushwa kwao kinyume na Matarajio.

**Tanbihi**

Dondoo limetolewa uk. 91.

**Hoja 5 x 2** **alama 10**

**Kutaja- 1**

**Mifano-1**

(XV) Sadfa - kitoto kinakufa na kijeremba kinapatikana papo hapo.



Scanned with CamScanner

(b) (i) Cizarina

i. Kupitia kwake tunatambua umuhimu wa utu. Anasimamia kituo cha Benefactor kinachowashughulikia watoto waliotelekezwa. (uk. 162) kitoto Riziki Immakulata kinaokolewa na kupelekwa katika kituo cha Benefactor.

ii. Anatumiwa kuonyesha uozo (ukatili) wa jamii. Anaeleza kuhusu mazoea ya baadhi ya binadamu kuwatupa watoto wachanga. Anasema kuwa binadamu amezika hadhi na utakatifu wa maisha ya mja katika kaburi la sahau (uk 162).

iii. Kupitia kwake tunatambua mchango wa baadhi ya taasisi zinazotoa huduma kwa madhumuni ya kuboresha maisha ya wanajamii. Anasimamia kituo cha Benefactor (uk 163).

iv. Anaendeleza/anachimuza maudhui ya ukiukaji wa haki za kibinadamu. Anakashifu watu ambao wamezika thamani ya binadamu.

v. Ni kiwakilishi cha uwajibikaji kuhusu utaratibu wa kisheria na wa kidini unaofuatwa katika kuwapangisha watoto (uk 163). /anasimamia kituo kinachowatunza watoto

vi. Anaangaza nafasi ya familia katika malezi (ya watoto wao na watoto wa kupanga). anamweleza Neema kuhusu kujitolea kwa familia katika kuwapanga watoto.

vii. Anawaelemisha wanajamii kuhusu suala na utaratibu wa upangaji wa watoto.

viii. Anaendeleza ploti. Kwenye kituo chake tunahadithiwa kuhusu maisha ya kitoto kilichookolewa na Neema. Kukikubali kitoto kilicholetwa na Neema kunabadilisha mkondo wa maisha ya kitoto hicho.

ix. Anaelimisha life za wahusika wengine kama Neema zote

**Hoja 5 x 1** **alama 5**

**Kutaja-1/2**

**Mfano -1/2**

(ii) Tila

i. Anadokeza suala la mabadiliko katika jamii na athari zakeyo kwa wanajamii. Kwa mfano, kubadilika kwa mfumo wa uzalishajimali, uongozi (kuwakumbatia wanawake katika uongozi). ( Rejelea Mazungumzo yake na baba yake(uk 38-44.)

ii. Anadokeza suala la mshikamano wa kifamilia. Palikuwa na uhusiano bora baina yake, nduguye na baba yao. Ridhaa anakumbuka wanawe Tila na Mwangeka walipokuwa wadogo walizoea kumkimbilia kila mara alipotoka kwenye shughuli zake za kikazi (uk 37).



Scanned with CamScanner

iii. *Anaangazia suala la jinsia. Anahimiza usawa katika jamii na katika uongozi. Mazungumzo baina yake na babake kuhusu wake kwa waume kupewa nafasi sawa (uk 39).*

iv. Kupitia kwake tunatambua kutowajibika kwa viongozi kutokana na kutotimizwa kwa matarajio ya wenyeji kuhusu ubora wa maisha yao (uk 40).

v. Anaangazia jinsi umaskini ulivyotamalaki katika jamii. Watu hawamudu mahitaji ya kimsingi; Watoto kufa kwa kukosa lishe bora, asilimia kubwa ya raia ambao hawamudu hata gharama ya matibabu (uk 41).

vi. Anadokeza uwepo wa ukengeushi katika jamii. Walio juu wamekengeuka na hawaoni/hawaelewi dhiki zinazowakumba wanyonge katika jamii (uk 43).

vii. Anachangia katika kubainisha hali tata zinazowakumba. Wahafidhina kama vile kuharibika kwa mazingira (kiangazi) na athari zake kwa jamii.

viii. Anaonyesha namna ubaguzi ulivyowaathiri Wahafidhina. (ix) Anaonyesha namna rasilimali za mataifa maskini zisivyowafaidi wenyeji bali hufaidi wawekezaji na baadhi ya nchi za kigeni.

ix. *Anaendeleza ploti.* Ridhaa anayakumbuka mazungumzo kati yake na Tila. Anaaangaza baadhi ya matukio ya awali.

x. Kupitia kwake, tunaangaziwa unafiki wa baadhi ya wafadhili ambao husingizia kuwa wanasaidia mataifa maskini kujiendeleza ilhali wao ndio hunufaika zaidi (uk 44).

xi. Anadokeza changamoto wanazopitia wafanyakazi kwenye kampuni za kuchimbua madini. Wanadhulumiwa kwa kupewa ujira mdogo (uk 44).

**Hoja 5 x 1** **(alama 5)**

**Kutaja- 1**

Mfano -1

xiii. Anaendeleza maudhui ya elimu.

(xiv) Anakuza sifa za Waluhika km mjadala wake na babake unambainisha Tila kama mluhika mwenye mawazo pevu. (uk 5-6)

(xv) Anaendeleza maudhui ya ungazi wa rasilimali/mazingira

(xvii) Anaendeleza maudhui ya haki na sheria. Keh amesema haziheshimiwi zitekelezwe (uk 45)

Zozote 5x1 = al 5

Kutaja ½

Mfano ½

For more visit : eazyarabic.com

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

4. (a)

(i) Msimulizi.

(ii) Anamrejelea Dadi.

(iii) Matukio yamo mawazoni mwa Msimulizi.

(iv) Huu ni ulinganuzi wa hali ya maisha ya Dadi.

(v) Baada ya kumchumbia Kidawa ambapo angekuwa na starehe ilhali ni kinyume.

**Hoja 4 x 1** **alama 4**

(Dondoo limetolewa uk. 56)

(b) Toni ya dhihaka/ stihizai/dhihaka

**Hoja 1 x 2** **alama 2**

**Kutaja-1**

**Mfano- 1**

c)

I. Dhana kwamba Kidawa anayavunja mashàrti ya ndoa kwa kumwendea kinyume linamkera Dadi.

II. Kidawa kumtia Dadi fedheha kwa kusimama na wanaume na kuamkiana na kuzungumza nao (uk 60).

III. Tabia ya Kidawa ya kupenda fasheni hii na ile na mavazi.

IV. Tabia ya Kidawa ya kujipodoa akiingia ndani (akirejea hata nyumbani. Mazoea ya Kidawa ya kujipodoa kila wakati yanamkera Dadi.

V. Anavyovalia Kidawa. Hajitandi kikamilifu. "… asiyetaka kuziba uso wala kifua chake." (uk 60). Haya yanamtia hisia za kutojiamini Dadi.

VI. Mtazamo wa Dadi- kuonekana na jamii, kuwa amedhibitiwa na mke wake pamoja na hisia kuwa amedhibitiwa na Kidawa kikweli anapofanya kazi za nyumbani. Dadi hana utulivu kutokana na haya.

VII. Utukutu wa Kidawa ambao unamfanya Dadi kuchelea kumwambia shauku aliyo nayo akihofia kuwa Kidawa atamrejesha kwenye "Masharti ya ndoa ya kisasa." (uk 61)



Scanned with CamScanner

XII. Hapendezwi na Kidawa kuchanuka kidhaa barabarani / nyumbani

XII. Kazi ya umetroni - Dadi hapendezwi na kazi ya Kidawa ya umetroni

VIII. Dadi anahisi kuwa "amejitia kitanzi' kwa kutia saini ya kukubali masharti ya kisasa. (uk 61), katika mkataba wa ndoa ya kisasa.

IX. Dadi ni mtumwa wa mapenzi kwani licha ya madhila yote anayopitia, anakiri kuwa bado anampenda Kidawa na anahofia kuwa kuvunjika kwa ndoa kutamwathiri mno (uk 62).

X. Dadi anadhihakiwa/anafanyiwa stihizai na baadhi ya wateja wake kama vile Bi. Zuhura anapomwuliza iwapo ana samaki wa kuuza au anao wa kwenda kumkaangia Bi. Kidawa (uk 62).

XI. Baadhi ya masharti yanamkera na kumhuzunisha Dadi kama vile kupata mtoto mmoja tu. (uk 61).

**Hoja 7 x 2** **(alama 14)**

**Tanbihi**

1. Misumari ya nyuki ni sitiari ya mambo yasiyopendeza/ jambo la kuhuzunisha/ jambo linaodhalilisha/ jambo la aibu.
2. Maana ijitokeze ili mtahiniwa atuzwe alama kamili.

5. (a)

(i) Ubakaji – Sara alifanyiwa ukatili na janadume moja ambalo lilimbaka alipokuwa anatoka masomoni.

(ii) Ubakaji unasababisha ujauzito wa kulazimishwa jambo ambalo Sara anahisi ni kuvunjiwa ujanajike na utu wake na kumharibia maisha.

(iii) Ujauzito unachangia uozo mwingine wa kutengwa sio tu na marafiki bali na wazazi pia. Katika ujauzito wake, Sara anafikiri jinsi atakavyotengwa na kila mtu-wa karibu na wa mbali.

(iv) Kuna ukandamiziaji wa jinsia ya kike. Sara anahisi kwamba alibakwa kutokana na imani ya jamii kuwa kiumbe mwanamke ni mnyonge. Anasema kuwa hata mama yake Sara anaudhika kuwa wanawake/wasio na nguvu wanazidi kudhulimiwa na wanaowadhulumu wanaachwa kunafasika. Aliyedhulumiwa ndiye anayaendelea kuathirika.

(v) Kuwaachia huru wabakaji/ kutowaadhibu wanaowadhalilisha wanawake.



Scanned with CamScanner

(vi) Ulipizaji kisasi – Sara anaishi na chuki linalosababishwa na kubakwa kwake. Ananuia kulipiza kisasi. Angetaka kumnasa na kumwadhibu yule nduli aitwaye babake mtoto wake.

(vii) Mauaji kutokana na watu kupigwa kitutu. Badala ya kuchukua hatua za kisheria za kuachia vyombo vya dola kukabiliana na wahalifu, jamii hii inachukua hatua mikononi mwake na kuwanyeshea washukiwa mvua ya matofali na kuwaua. Bakaji linauawa na watu wenye ghadhabu.

(viii) Udaku – Ni jamii inayoshiriki umbea na udaku. Sara anachelea vile majirani wataanza kumsema watakapotambua kuwa ni mjamzito.

**Hoja 5 x 2 = 10**

**Kutaja 1**

**Mifano 1**

***Tanbihi***

Hoja ijadiliwe kikamilifu na kutolewa mifano ili apate alama 2.

(b)

(i) Wazazi wanawaelimisha watoto wao – Biti Kidebe alimpeleka skuli Mashaka. Hivyo kumpa mbinu za kujitegemea. /Waridi kufunzwa. hivyo kumpa mbinu za kujitegemea.

(ii) Wazazi wanawalea watoto kwa kuwapa mahitaji ya kimsingi. Biti Kidebe alimlea Mashaka.

(iii) Wazazi wanawafunza watoto uwajibikaji. Mashaka aliwajibika katika kazi mbalimbali ili kusaidia katika kuikimu familia.

(iv) Wazazi wanapaswa kutoa ushajiri na uelekezi kwa wana wao. Mashaka na Waridi wanajikuta wakishiriki mapenzi wakiwa wachanga bila ya kufahamu wajibu unaoandamana na tendo hilo na kuishia kulazimika kuoana wakiwa wachanga.

(v) Wazazi wanawapa wana wao mbinuishi/ stadi za kukabiliana na maisha. Mashaka anajifunza shughuli za ukulima.

(vi) Kufunza matumizi yafaayo ya raslimali ili kujikimu. Biti Kidebe na Mashaka wanalima vishamba vyao na kupata mahitaji ya kila siku.



Scanned with CamScanner

For more visit : eazyarabic.com

(vii) Kufunza umuhimu wa mahusiano mema ya kijamii/umuhimu wa utubora. Biti Kidebe anamchukua na kumlea Mashaka licha ya kuwa si mwana wake.

(viii) Kufunza umuhimu wa kuuwekea msingi mustakabali wa maisha. Biti Kidebe anaweka akiba anayotoa ili kuwasaidia wakati wa upungufu.

(ix) Wanawahimiza kudumisha mila na utamaduni. Mzee Rubeya na Shehe wanadumisha mila na utamaduni kwa kuwaoza Mashaka na Waridi wanapoanza kujiingiza katika mapenzi.

(x) Kuwasaidia wana wao wanapokabiliwa na matatizo. Waridi anarejea kwao na watoto wake ili kuauniwa wakati wa shida.

(xi) Wanazorotesha hali ya maisha ya watoto wao kwa kuwaoza bila kufikiria mustakabali wao. Mashaka na Waridi wanaishia kukaa katika mazingira duni. Wanaomba nafasi kwa jirani ili watoto wao wapate mahali pa kulala.

(xii) Wanawakosesha wana wao usalama. Watoto wanalazimika kuchezea nje baba yao anaporejea nyumbani.

(xiii) Wanawadhalilisha watoto wao. Mashaka na Waridi wanaomba nafasi ya watoto wao kulala huko kwa jirani.

**Hoja 5 x 2 = 10**

**Kutaja 1**

**Mfano 1**

**Tanbihi**

Hoja ijadiliwe kikamilifu na kutolewa mifano ili apate alama 2.



Scanned with CamScanner

## SEHEMU D: USHAIRI

6. (a) Ujumbe

(i) Mtu mbaya/asiye na heshima hana msimamo.

(ii) Asiye na heshima huona aibu kwa kukosa heshima.

(iii) Mtu mbaya/mwenye kukosa heshima anafaa kuepukwa.

(iv) Mtu mbaya ukiwa na shida atakukimbia peupe ubaki kujuta.

(v) Mtu asiye na heshima hujiaibisha/hujidhalilisha kwa wengine..

(vi) Asiye na heshima hawasaidii watu.

(vii) Watu wa aina hii ni kawaida kuwapata.

(viii) Mtu asiye na heshima ni hatari.

(ix) Asiye na heshima habagui analonena( Hana heshima ya neno)

**Hoja 4 x 1 = alama 4**

(b) Nafsineni ni
- Mshauri
- *Mwelekezi*
- Anayetahadharisha/anayeonya
- Anayetoa nasaha

**Hoja 1 x 2 = alama 2**

(c) Uhuru wa kishairi ulivyotumiwa

(i) Miundo ngeu ya kisintaksia/kuboronga sarufi/ kufinyanga lugha – mfano wake tazama – tazama mfano wake kama popo mwendo wake – mwendo wake kama popo. Mshairi amebananga lugha ili kuleta urari wa vina

*(ii)* Udondoshaji wa maneno ili kuleta urari wa mizani (Ubeti 2:1) ya ndege na wanyama, badala ya: ya ndege na ya wanyama.
Hudai ndege wenzake – hudai ndege ndio wenzake.

*(iii)* Ufupishaji/inkisari ili kuleta urari wa mizani kamaye – kama yeye ( Ubeti 2:4).

*(iv)* Urefushaji/mazida ili kuleta urari wa mizani / vina hanayo – hana ( Ubeti :2); hutendekana – hutendeka ( Ubeti 5:3).

**Mifano 3 x 2 = 6**

**Kutaja 1**

**Umuhimu – 1**



Scanned with CamScanner

d) urudiaji ulivyotumiwa

i) Urudiaji (takriri) wa sauti k.v. (ke), (no) kuwa alama ya kipumuo cha shairi/ kulipa shairi muonjo wa kimuziki..

ii) Urudiaji wa maneno; heshima, hiana -kutilia mkazo hoja husika/kusisitiza.

iii) Usambamba – miundo inayofanana ya kisintaksia inatumiwa kuleta mvuto katika shairi.

Hana masikilizano Ubeti 2:3

Hana heshima ya neno Ubeti 3:3

2 x 2 = 4

**Kutaja-1**

**Dhima-1**

e) Tamathali za usemi katika ubeti wa kwanza na wa pili.

i. Tashbihi – kama popo mwendo wake ( Ubeti 1:2).

ii. Uhaishaji – siku ya ndege na wanyama kupatana (2:1).

**2 x 1 = 2**

**Kutaja ½**

**Mfano ½**

f) Ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari

Mtu mwenye hiana ni mbaya na ukiwa naye utajilaumu. Iitokea kwamba dunia itakutatiza mtu huyo atakutupa mchana peupe. Haya ni mambo yanayotupata na yanayotendeka.

**Hoja 4 x ½ =** **alama 2**

7. (a)

(i) Analetea mazingira.

(ii) Mito kuchafuliwa na watu wanaofanyia usafi huko.

(iii) Hakuna kilicho safi.

(iv) Watu hupitia mto uliochafuliwa bila kujali.



Scanned with CamScanner

For more visit : eazyarabic.com

(v) Mto kusafishwa siku moja ili kuufanya mji upendeze.

(vi) Tunahitajika kutetea uhifadhi wa mazingira-Ningekuwa *mimi ningepaza* sauti;punguzeni bughudha.

(vii) Linakashifu unafiki- watu kuukosha mji mwakani na hali hawajali kuuhifadhi mto.

(viii) Linalalamikia ukosefu wa uwajibikaji- watu wanaubebesha mto uchafu ili wenyewe wapate kuwa safi/ wanaelekeza uchafu kwenye mto.

**Hoja 5 x 1 =** **(alama 5)**

(b)

(i) Miundo ngeu ya kisintaksia/ Kuboronga sarufi/Kubananga lugha – makubwa kushuhudia – kushuhudia makubwa.

(ii) Inkisari – Safika – kusafika.

**Hoja 2 x 1 =** **(alama 2)**

(c)

(i) Tashihisi – Mto kuona mengi, mto kushuhudia makubwa, mto kutambaa, mto kuwa kimya, mto kuoshwa.

(ii) Swali la balagha – Hamjui mto husafisha dhambi?
- Mto hukoshwa kwa sabuni?

(iii) Kinaya - Kufumbia jijo macho.
- Kufanyia usafi mtoni huku wakiuchafua.
- Kufanyia usafi mto huku nia yao ikiwa kuufanya mji upendeze.
- Kufanya usafi wa mto wa siku moja.
- Mto kuona mengi hali hausemi chochote.
- Mto unaoshwa badala ya wenyewe kutakasa dhambi.

**Hoja 3 x 1 =** **(alama 3)**

**~~Kutaja 1~~**

**Mifano-1**

(d)



Scanned with CamScanner

(d)

(i) Urudiaji neno – mto, jiji

(ii) Usambamba – wanaolivuka bila fahamu

Wanaolima bila kujali

**Hoja 2 x 1 =** **(alama 2)**

(e) **Nafsineni**

(i) Mtetezi wa mazingira

(ii) Anayelalamikia uchafuzi wa mazingira

(iii) Mtetezi wa usafi wa mto

(iv) Anayepinga uchafuzi wa mazingira/mto

(v) Mtu wa kizazi cha sasa.

**Hoja 1 x 1 =** **(alama 1)**

(f)

(i) Mwendo – utambao, wanaolivuka, kilichopita

(ii) Uoni – wanalifumbia macho.

- nionavyo
- ulioona

(iii) Hisi – nalilia mazingira.

(iv) Usikivu – ningepaaza sauti

**Hoja 3 x 1** **(alama 3)**

**Kutaja ½**

**Mifano ½**

(g)

(i) Kulalamika – nalilia mazingira yetu/hakuna kilicho safi.

(ii) Dhihaka/kubeza – najua mwakani …

**Hoja 1 x 2** **(alama 2)**

(h) Najua kwamba watakuja mwakani kuusafisha mto kwa siku moja, ila madhumuni yao ni kuufanya mji upendeze wala si kuusafisha mto.

**Hoja 4 x 1/2** **(alama 2)**



Scanned with CamScanner

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a)(i) Hurafa – wahusika wanyama

**1 x 2 = 2**

**Kutaja – 1**

**Mfano – 1**

(ii)

I. "Dayolojia za wahusika – Sungura anazungumza na Nungunungu.

II. Uzungumzi nafsia – Nungunungu anajisemea- Simtarajii ndugu yangu huyu aniendee kinyume/.

III. Swali la balagha – Itatokeaje anisaliti baada ya muda wote huu?

IV. Kuzungumza moja kwa moja na hadhira ili kuibua taathira ifaayo – Basi mjukuu wangu.

V. Upenyezi wa mtambaji – Unajua tena mjukuu wangu kauli za mwenye hila haziaminiki.

VI. Chuku -maghala yalishiba yakatapika nafaka.

VII. Tashihisi – kiangazi kilizidi kung'ata.

VIII. Matumizishirikisha hadhira kwa kuuliza maswali- Mjukuu wangu ingekuwa wewe ungemfanyia nini rafiki yako huyu wa dhati?

IX. Matumizi ya lugha sahili.

X. Matumizi ya fomyula ya ufunguzi na ya kuhitimisha/ tamati.

XI. Taharuki/lugha inayojenga taharuki.

XII. Muundo sahili wa hadithi.

**6 x 1 = 6**

(iii)

i. Ukulima – Nungunungu alikuwa na nafaka/maghala ya nafaka.

ii. Uwindaji – Fisi anamezwa na msitu kutafuta mizoga/anajiulia.

iii. Ufugaji – **Mbuzi** wangu wale majani mabichi/kumiliki mbuzi.

**3 x 1 = 3**

iv) Umuhimu wa fomyula ya mwisho

I. Kuashiria mwisho wa ngano.



Scanned with CamScanner

vi- kutoa funzo kwa mjukuu wangu ingekuwa wewe.
vii. kumpisha mtambaji anayefuata
viii. kuipisha shughuli inayofuata
ix. kuipa hadhira changamoto/swali la kutafakari kama ungekuwa wewe ungefanya nini katika yao hapa dhahi:

II. Kuitoa hadhira kwenye ulimwengu wa fantasia hadi ulimwengu halisi.

III. Kuonyesha mwisho wa mgogoro/suala linaloangaziwa. Fisi anaishikwa.

IV. Ni kitulizo kwa hadhira – imejua hatima ya fisi – ameadhibiwa.

V. Kusawiri jamii ambamo utungo unapatikana – ni wafugaji.

Za kwanza **4 x 1 = 4**

(b)

(i) Kuirithisha fani yenyewe ya utambaji kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

(ii) Kukifanyia utafiti ili kubainisha sifa za uwasilishaji wazo na kuzihifadhi.

(iii) Kuzihifadhi kwenye maandishi.

(iv) Kujifunza/kuzifunza shuleni.

(v) Kuzitamba mara kwa mara.

(vi) Kuzihifadhi kwenye video ili kuhifadhi sifa za uwasilishaji kama vile sauti/kidatu, na miondoko.

(vii) Kutafitia vyanzo vya kudidimia kwazo ili kuvidhibiti/ kvitatua.

(viii) Kuandaa mashindano ya utambaji wa ngano ili kurithisha utambaji wazo kutoka kizazi hadi kingine/ kuwafanya vijana wavutiwe nazo..

(ix) Kufadhili utafiti kuhusu ngano.

(x) Kushirikisha wageni waalikwa katika ujifunzaji wa ngano/ kuzifunza kwa mitindo anuwai ili kuwafanya wanafunzi wavutiwe nazo, na kuziendeleza.

(xi) Kuzitumia kufunzia masomo mengine na stadi nyingine kama vile kusikiliza na kuzungumza.

(xii) Kuandaa vipindi vya redio au runinga na kuwaalika mafanani stadi kutamba ili kuwa vielelezo.

**5 x 1 = 5**

xiii. Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wake
xiv. Wizara ya elimu kuweka sera zinazohimize na kulinda utambaji na uhifadhi wa ngano.

Za kwanza 5 x 1 = alama 5



Scanned with CamScanner